



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI



TAARIFA KWA UMMA.

YAH: UFAFANUZI WA VYETI VITOЛЕWAVYO NA BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI (PSPTB)


DODOMA, 22 NOVEMBA, 2024

Napenda kukufahamisha kuwa Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) ilianzishwa kwa sheria namba 23 ya mwaka 2007 ikiwa chini ya Wizara ya Fedha. Pamoja na shughuli nyingine Bodi huratibu mafunzo ya kitaaluma na kutoa mitihani, kutambua ufaulu na kutunuku vyeti kwa watahiniwa wake vinavyotambulika katika mifumo ya ajira kama ifuatavyo;

2. Vyeti vya *National Store keeping Certificate (NSC), Procurement and Supplies Management Foundation Certificate (PSMFC) na Professional Diploma in Procurement and Supply Management (PDPSM)* ni vyeti vya kitaaluma ambavyo mwanataaluma hutunukiwa baada ya kupata mafunzo ya muda mrefu ya kitaaluma na kufaulu mitihani husika kisha kusajiliwa kwenye **“Full Technician” au Technician Category**. Wahitimu mwenye vyeti hivi hulinganishwa na mhitimu mwenye cheti cha stashahada yaani **“Diploma”** kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali na humwenzesha mhusika kufanya kazi kama msaidizi katika eneo la ununuzi, ugavi au usimamizi mali (*Assistant Procurement, Supply or Asset management*).
3. Vyeti vya *Graduate Professional in Procurement and Supply Management* ambavyo ni vyeti vya kitaaluma vinavyotunukiwa mwanataaluma baada ya kupata mafunzo ya muda mrefu ya kitaaluma na kufaulu mitihani husika kisha kusajiliwa kwenye **“Graduate Professional Category”**. Pia mtahiniwa mwenye hati za ufaulu kwa mhitimu wa ngazi ya tatu ya mafunzo na mitihani ya kitaaluma yaani (*Professional Stage III*), Wahitimu mwenye hati na vyeti hivi wanakuwa nahadhi sawa na wahitimu wenye vyeti vya Shahada kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali na kumwenzesha mhusika kufanya kazi kama Afisa katika eneo la ununuzi, ugavi au usimamizi mali. (*Procurement Officer, Supplies or Asset management Officer*).

4. Cheti cha kitaaluma cha shahada ya juu ya ununuzi na ugavi "The Certified Procurement and Supplies Professional (CPSP)", "The Certified Supplies Professional (CSP)" au "The Certified Procurement and Supplies Professional in Tanzania (CPSP-T) – ni vyeti vya kitaaluma ambavyo mwanataaluma hutunukiwa baada ya kupata mafunzo ya muda mrefu ya kitaaluma na kufaulu mitihani husika kisha kuweza kusajiliwa kwenye "**Approved or Authorized Categories**" Kulingana na muongozo wa usajili kitaaluma. Wahitimu mwenye vyeti hivi hulinganishwa na wahitimu mwenye cheti cha kitaaluma cha *Post Graduate professional practice Studies* kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali na kumwenzesha mhusika kufanya kazi kama Afisa, mwandamizi ama afisa mkuu na kuweza kuwa mkurugenzi wa idara, mkuu wa kitengo, mkuu wa sehemu n.k. katika eneo la ununuzi, ugavi au usimamizi mali (*Procurement, Supplies or Asset management Section, Unit, Department, Division or Directorate*).

5. Asante kwa ushirikiano wako na Bodi inakuahidi kwamba iko tayari wakati wote kuendelea kutoa ufanuzi wowote utakaohitajika.



Godfred B. Mbanyi
MKURUGENZI MTENDAJI

GBM/jje.

Tambukareli